

Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 APRILI, 2026 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 11-20 APRILI, 2026.

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA TAREHE 01-10 APRILI, 2026.

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kudhoofika. Hali hii ilisababisha ukanda mvua kusogea kidogo kuelekea kaskazini na kuendele kuwepo katika maeneo mengi ya nchi na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika baadhi ya maeneo.

Aidha, upepo wenye unyevunuevu uvumao kutoka katika misitu ya Congo na kuelekea katika maeneo ya magharibi mwa nchi, nyanda za juu kusini magharibi na kanda ya kusini uliimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 APRILI, 2026.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo mengi ya nchi. Pia, vipindi vya mvua kubwa viliripotiwa katika maeneo ya ukanda wa pwani, kanda ya kusini na magharibi mwa nchi.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 11-20 APRILI, 2026.

2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 11-20 APRILI, 2026.

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua kusogea kidogo kuelekea kaskazini na kuendelea kuwepo katika maeneo mengi ya nchi na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika baadhi ya maeneo. Aidha, upepo wa bahari wenye unyevunuevu uvumao kutoka mashariki na kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani unatarajiwa kuimarisha zaidi mifumo

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

isababishayo mvua katika maeneo hayo.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 APRILI, 2026.

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara): Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro): Mvua zinatarajiwa katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Vipindi vya mvua kubwa zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Vipindi vya mvua kubwa zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Imetolewa na:

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz